## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI

**18 JUNI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

### KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI – TAREHE 18 JUNI, 2026

**I. DUA:**

**II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

**III. MASWALI YA KAWAIDA:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

**620. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Kidimu - Mpiji ili kutatua changamoto ya Wakazi wa Pangani Kibaha kuvuka Mto Mpiji kuelekea Kibamba.

**621. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Namwinyu Wilayani Tunduru.

**622. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya au Zahanati katika Kata ya Mbugani yenye wakazi zaidi ya 20,000.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**623. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, zipo athari za kijamii kwa wenza wa Watumishi kuishi mbali na Watoto wao.

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

**624. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mwongozo na uratibu wa kusimamia fedha za mikopo kwa Wafanyabiashara ndogondogo ili kudhibiti upotevu wa fedha hizo.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**625. MHESHIMIWA MARIAM MADALU NYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa Mafunzo ya Ufugaji wa Samaki na Kuku kwa Vijana na Wanawake Mkoa wa Ruvuma.

## WIZARA YA MAJI:

**626. MHESHIMIWA ARIF SULEIMAN PREMJI (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji Mwaka 2025/26 umefikia asilimia ngapi ikiwa Shilingi Bilioni 943 zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## WIZARA YA KILIMO:

**627. MHESHIMIWA LUTENGANO GEORGE MWALWIBA (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusimamia ubora wa Zao la Parachichi mashambani ili kuzuia migogoro kati ya Wanunuzi na Wakulima.

## WIZARA YA UJENZI:

**628. MHESHIMIWA TWAHA SAID MWAKIOJA (MKINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini taratibu za kumpata Mkandarasi zitakamilika ili ujenzi wa Barabara ya Maramba - Mtapwa Km 10 uanze mwaka huu wa Fedha.

**629. MHESHIMIWA FAGASON ARON NKINGWA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Masumbwe, Mbogwe, Lulembela kwa kiwango cha lami.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**18 JUNI, 2026** **KATIBU WA BUNGE**